

DISTINCTION GREDI YA SITA KPSEA ASSESSMENT



MONITORING LEARNER'S PROGRESS

GREDI YA SITA - 2023

KISWAHILI

6

Muda: saa 1

PREMIER

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.

Hapo zamani za kale, katika ulimwengu wa wanyama, paliishi Nyati na Ngiri. Wawili hao walikuwa na familia zao. Kila mmoja alikuwa na nyumba yake, mke pamoja na watoto. Ngiri alikuwa na watoto sita naye Nyati alikuwa na watoto watano. Walifuga wanyama kama vile mbuzi, ng'ombe, kondoo na ngamia. Wanyama hao waliwapa faida ya maziwa na wakati fulani kuwafanyia kazi. Tofauti kubwa iliyokuwapo ni kuwa Nyati alipenda sana kuwapeleka wanawe shuleni. Kila jua lilipochochoza, aliandamana



na watoto wake hadi shuleni. Baadaye aliwachukua jioni na kuwarudisha nyumbani. Ngiri naye alikataa kabisa kuwapeleka watoto shuleni. Alienda nao shambani kila wakati. Watoto na mkewe walijaribu kumwambia umuhimu wa masomo lakini alikataa kuwasikia.

Baada ya miaka kadhaa, watoto wa Nyati walikamilisha masomo. Tofauti moja iliyoonekana ni kuwa watoto wa Nyati walikuwa na tabia nzuri wakilinganishwa na wale wa Ngiri. Walikuwa wenye heshima kwa wenzao na kufuata sheria. Pia walikuwa wenye ushirikiano mno. Vilevile, wengi wao walikuwa wamegundua talanta zao wakiwa shuleni. Kwa hivyo waliweza kuendeleza talanta hizo. Hatimaye, watoto wa Nyati walipata kazi kwa haraka sana. Watoto wa Ngiri walimlaumu sana baba yao. Hapo ndipo Ngiri alipogundua kuwa elimu ina manufaa sana.

1. Kila mnyama alikuwa na vitu vifuatavyo **isipokuwa**;
A. nyumba
B. mke
C. watoto
D. msitu
2. Gani si faida ya elimu kulingana na kifungu?
A. kujifunza ushirikiano
B. kutambua talanta
C. kuwa na tabia nzuri
D. kulaumu wazazi
3. Unadhani ni kwa nini Nyati aliandamana na wanawe hadi shuleni na kuwachukua jioni?
A. hawakujua shule ilipokuwa
B. alitaka wafike haraka
C. alitaka kuwapa ulinzi
D. alitaka wasome kwa bidii
4. Kwa nini Ngiri hakuwapeleka watoto wake shuleni?
A. walikuwa wengi
B. shule ilikuwa mbali
C. hakuwa na pesa za kulipa karo
D. hakuwajua umuhimu wa elimu
5. Ni kweli kuwa elimu iliwasaidia watoto wa Nyati katika njia gani?
A. kuwa na maadili, kupata kazi
B. kupita mihani, kuwa na tabia
C. kuonekana wazuri, kupata kazi
D. kupata kazi, kupita mihani
6. Nyati alikuwa mzazi mzuri kwa sababu gani?
A. Alicheza na watoto wake
B. Aliwaonyesha shule
C. Alihakikisha kuwa wamesoma
D. Aliwapa chakula na nguo

7. Umejifunza nini kutokana na kisa hiki?
 A. Nyati ni mnyama mwerevu
 B. Elimu ni muhimu maishani
 C. Ngiri ni mnyama mjinga
 D. Watoto wa ngiri huteseka

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Uchochole twakupinga, lazima tutakushinda,
 Mipango tumeipanga, na mimea tutapanda,
 Ushuru tutauchanga, uchumi wetu kuunda,
 Ni lazima tuungane, utajiri tutapata.

Wanyamapori kutunza, watalii watakuja,
 Shirikiana twaanza, tutapatiwa faraja,
 Kuwapenda wetu wenza, kuheshimu wote waja,
 Ni lazima tuungane, utajiri tutapata.

8. Vina vya kati vya ubeti wa pili ni vipi?
 A. nga B. nda
 C. nza D. ja
9. Kuwatunza wanyamapori kuna faida gani kulingana na shairi?
 A. huleta ushirikiano
 B. huvutia watalii
 C. huleta faraja
 D. hufanya tuungane
10. Mshororo wa kwanza katika ubeti wa kwanza una mizani mingapi?
 A. 16 B. 8
 C. 2 D. 64
11. Badala ya neno **uchochole**, mwandishi wa shairi angetumia neno gani lenye maana sawa?
 A. shida B. pesa
 C. afya D. umaskini

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.

Lishe bora ni muhimu kwa afya ya mwili. Lishe bora inajumuisha vyakula kama vile nafaka, maziwa, samaki, mboga na matunda. Vyakula hivi huwa na wanga, protini, vitamini pamoja na madini. Tahadhari, vyakula visiwe na mafuta, chumvi au sukari kwa wingi. Wanga huwa chakula cha kuongeza nguvu mwilini. Mwili ukiwa na nguvu, misuli hufanya kazi vizuri. Vyakula kama vile viazi vitamu, ndovi, mihogo na nafaka ndivyo vyenye wanga. Vyakula kama vile samaki, maziwa na maharagwe huwa na protini. Protini hujenga mwili. Vitamini ni virutubisho muhimu sana vinavyopatikana katika vyakula kama vile machungwa, tikitimaji, mchicha na mrenda. Vitamini hukinga mwili dhidi ya maradhi. Maji ni muhimu sana kwa afya ya mwili na akili. Mtu anafaa anywe maji bilauri nane kwa siku. Waama maji ni uhai.

Mazoezi ya mwili huzuia magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama vile saratani, mshtuko wa moyo na kisukari. Mbali na hayo, mazoezi husaidia misuli kuwa imara, viungo vya mwili kuwa vyepesi, mifupa kuwa na nguvu, kuboresha utendakazi wa akili, kujiepusha na tabia za kupotosha, kuboresha afya ya ngozi na kupata usingizi. Kwa hivyo, mazoezi huboresha afya.

Mazingira safi huboresha afya ya mwili. Mtu akiishi katika mazingira safi huepukana na magonjwa ya kuambukizwa kama vile kipindupindu, kichocho, malaria, malale na homa ya matumbo. Vilevile, mazingira safi hurahisisha kufanya kazi. Mazingira machafu ni makazi ya nzi na wadudu waenezao magonjwa. Mazingira safi ni muhimu katika ufanyaji kazi goyote ile.

12. Kulingana na kifungu, ugonjwa gani ambao hauwezi kuzuilika kwa kufanya mazoezi?
 A. saratani
 B. mshtuko wa moyo
 C. kisukari
 D. kipindupindu
13. ili kuepuka wadudu kama vile nzi, mtu anashauriwa kufanya nini?
 A. Kuzingatia usafi
 B. Kupata lishe bora
 C. Kufanya mazoezi
 D. Kula chakula safi

14. Orodha gani inayoonyesha mfano wa lishe bora kulingana na kifungu?
 A. ugali, nyama, chai
 B. wali, maharagwe, embe
 C. chipsi, kuku, soda
 D. chapati, nyama, viazi
15. Kifungu kinashauri kuwa mtu anafaa kunywa maji;
 A. yaliyochemshwa.
 B. bilauri zaidi ya nane kwa siku.
 C. mengi sana kila siku.
 D. bilauri nane kwa siku.

Jaza nafasi zilizoachwa kwenye kifungu kifuatacho kwa kuchagua jibu sahihi.

Mwanzele na dada yake hupenda kusoma na kusakura mtandaoni. 16 kuanza kusakura, wao huenda kwa mzazi wao ili kuomba 17. Wao hufuata maagizo 18 na mzazi wanaposakura mtandaoni. 19 wakatoa habari za kibinafsi kwa mtu wasiyemjua mtandaoni. Hakika, wanaelewa kuwa 20.

16. A. Badala ya B. Kabla ya C. Baada ya D. Baadaye
17. A. msamaha B. adhabu C. radhi D. idhini
18. A. wanayopewa B. wanayopeana C. anayopewa D. wanayotoa
19. A. Wanaweza B. Hawawezi C. Hawakuweza D. Hawataweza
20. A. mtoto umleavyo ndivyo akuavyo B. asiyesikia la mkuu huvunjika guu
C. mgaagaa na upwa hali wali mkavu D. polepole ndio mwendo

Kuanzia nambari ya 21 -30, jibu swali kulingana na maagizo.

21. Tambua ukubwa wa;
Mti ule una ndege wengi.
A. Jiti lile lina madege mengi.
B. Jiti lile lina majidege mengi.
C. Jiti ule una madege wengi.
D. Vijiti vile vina videge vingi.
22. Maneno yafuatayo yatafuatana vipi katika kamusi?
i. chungwa
ii. chungu
iii. chunguza
iv. chungu
A. iv, iii, i, ii
B. ii, iv, iii, i
C. iii, i, ii, iv
D. i, ii, iv, iii
23. Chagua jibu ambalo **halijalinganisha** kitenzi na kinyume chake kwa usahihi.
A. anika – anua
B. funga – fungua
C. tega – tegua
D. chimba – chimbua
24. Tambua orodha iliyo na nomino za dhahania.
A. umati, thurea, bumba
B. maji, mafuta, chai
C. kiti, gari, nyumba
D. hasira, furaha, wasiwasi
25. Yafuatayo ni maamkuzi **isipokuwa**;
A. masalheri
B. chewa
C. buriani
D. shikamoo
26. Chagua sentensi iliyo katika hali ya mazoea.
A. Mwanabiashara huyo amelipa ushuru wote.
B. Wimbo wa taifa huimbwa kila siku ya Jumatatu na Ijumaa.
C. Juma anakula matunda na mboga za kienyeji.
D. Nitakununulia mipira ya kufanyia mazoezi.
27. Chagua ukanusho wa;
Anasoma kwa kasi inayofaa.
A. Hasomi kwa kasi inayofaa.
B. Hakusoma kwa kasi inayofaa.
C. Hujasoma kwa kasi inayofaa.
D. Sitasoma kwa kasi inayofaa
28. Chagua kitenzi kilichonyambuliwa katika kauli ya kutendeka.
A. pika
B. fika
C. weka
D. vunjika
29. Orodha gani iliyo na nomino za ngeli ya KU – KU?
A. sokoni, nyumbani, bustani
B. kufuli, kusoma, kuku
C. kunguru, kuku, kurumbiza
D. kuimba, kutembea, kuandika
30. Ikiwa jana ilikuwa Alhamisi, kesho itakuwa lini?
A. Ijumaa
B. Jumamosi
C. Jumapili
D. Jumatatu

INSHA

Andika insha ya wasifu kuhusu,

DARASA LETU